BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Sita – Tarehe 06 Disemba, 2023.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Afya:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa ajili ya Ununuzi, Utengenezaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa ajili ya Ununuzi, Utengenezaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

60. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

    Ni changamoto gani ambazo Diaspora wanakutana nazo katika kuweka miradi mbali mbali ya kimaendeleo na kwa namna gani Serikali inawapatia ushirikiano wa kutosha.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

47. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Baadhi ya vikundi vilivyosajiliwa rasmi na watu wenye mahitaji maalum kwa mfano wenye matatizo ya usikivu na uoni, wamejaribu kuitika katika fursa za mikopo nafuu ya Dkt. Hussein Mwinyi kupitia uwezeshaji, kwa lengo la kujikimu na kujikwamua kiuchumi.

    (a) Je, ni kwa nini vikundi hivi vinashindwa kupatiwa mkopo huo licha ya kukamilisha taratibu zote zinazostahiki.

    (b) Kupitia mikopo hiyo, je Wizara yako haioni kwamba ipo haja ya kutoa kipaumbele kwa watu wenye mahitaji maalum kwa kuwa wameweza kuthubutu katika kujianzishia miradi yao.

72. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    (a) Je, ni kwa kiasi gani asilimia nne (4%) inayotolewa na Halmashauri ya Magharibi "B" kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum inawanufaisha walengwa.

    (b) Je, ni vikundi vingapi vya watu wenye mahitaji maalum vilivyopata usajili rasmi vinanufaika na mgao huo.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

17. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

    Kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya vitendo vya udhalilishaji nchini ikiwemo ulawiti. Na kwa kuwa jambo hili litalipelekea taifa letu kupoteza sifa, muelekeo na uasili wake.

    (a) Je, ni vijana wangapi wa kiume tayari wameathirika na janga hili kwa kila Wilaya na wamepoteza uasili wao.

    (b) Kwa kushirikiana na Wizara ya Afya. Je, Wizara yako imejipanga vipi kutafuta tiba (dawa) za kurejesha uasili wa vijana hao walioathirika.

(c) Je, ni hatua zipi zitakazochukuliwa na Wizara yako katika kupunguza vitendo hivyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

21. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hatua nzuri na juhudi kubwa iliyofikia katika kuimarisha sekta ya elimu visiwani Zanzibar. Serikali inaendelea na ujenzi wa skuli za ghorofa katika maeneo mbali mbali, lengo ni kuwawezesha wanafunzi wetu kusoma katika mazingira bora na yenye ufanisi zaidi.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya kufundishia vinapatikana katika skuli hizo.

(b) Ni ipi mikakati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuhakikisha kwamba, walimu na wanafunzi wanaosoma katika skuli hizo wataweza kuvitumia vifaa hivyo kwa ufanisi mkubwa hasa tukizingatia teknolojia inaendelea kukuwa siku hadi siku.

45. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na maboresho ya mitaala ya mfumo wa elimu katika vipindi mbali mbali kutokana na haja ya mabadiliko yanayojitokeza ya kiteknolojia, kiuchumi na kijamii.

Je, ni maboresho mangapi ya mfumo wa elimu kupitia mitaala yamefanyika mpaka sasa na yamepishana kwa vipindi gani.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

35. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA Ameir (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Je, Wizara yako inatumia mikakati gani ya kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kuvuka katika hatua ya kati na kufikia hatua ya juu ya uvuvi wa bahari kuu.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

46. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

    Nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendeleza azma njema za ujenzi wa nyumba bora na za kisasa kwa wananchi wa Zanzibar, akifuata nyayo halisi za marehem Shekh Abeid Aman Karume kuona kila Mzanzibari anaishi katika mazingira mazuri.

    (a) Je, ni nyumba ngapi za makaazi ya wananchi zinatarajiwa kujengwa kwa kipindi cha miaka miwili ijayo.

    (b) Ni yepi matarajio ya ujenzi wa nyumba kama hizo maeneo ya vijijini.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

66. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    (a) Ni miji gani duniani ya hifadhi ya dunia inayofanana kwa ukaribu na mji Mkongwe wa Zanzibar.

    (b) Je, ni misikiti na makanisa mangapi yanayopatikana ndani ya mji huu wa hifadhi ya urithi wa dunia na kwa kiasi gani uwepo wa nyumba hizo za ibada na nyenginezo unaakisi muendelezo wa historia ya uvumilivu wa kidini Zanzibar.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

68. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Kwa kiasi gani watendaji wa Shirika la Bandari wanawashirikisha wataalamu wa mambo ya kale kwenye miradi ya kimkakati inayoendelea eneo la kihistoria la Mangapwani ili kuweza kuilinda na kuihifadhi historia yetu.

**Wizara ya Afya:**

13. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Kwa kuwa Wizara imeingia mikataba na makampuni mbali mbali katika kuziendesha na kutoa huduma katika hospitali zetu ikiwemo Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

    (a) Je, kuna uhakika gani wa kuendelea kwa huduma zinazotolewa na Kampuni hizo (out sources).

    (b) Endapo kampuni itavunja mkataba, Serikali itajipanga vipi kutoa huduma za Afya kwa haraka.

    (c) Kwa kuwa kampuni hizo zipo kibiashara zaidi. Je, tathmini ya Wizara yako iko vipi kwa kipindi hiki walichofanya kazi hasa katika ubora wa huduma na gharama za matibabu.

14. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Kwa kuwa vifo vingi hutokea baada ya mama kujifungua na kumekuwepo na taarifa nyingi za kitakwimu zinazotolewa mwaka hadi mwaka.

    (a) Je, ni kipindi gani kitaalamu mwanamke huhesabiwa amefariki uzazi sambamba na watoto wanaozaliwa.

    (b) Je, vifo vingapi vya kipindi cha siku arubaini (40) vilivyotokea katika mwezi wa Januari hadi Oktoba, 2023.

    (c) Je, ni ipi kauli kitaalamu katika kupunguza vifo hivi.

55. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Maradhi ya kupooza viungo na mwili kwa ujumla yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku.

    (a) Ni nini hasa kiini cha maradhi haya.

    (b) Ni upi mpango mkakati wa kuyatokomeza maradhi ya kupooza.

(c) Kwa nini hata watoto wadogo wamekuwa waathirika wa maradhi haya kwa miaka ya hivi karibuni.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

77. Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir (Jimbo la Mwanakwerekwe): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

    Kwa sasa ni bidhaa gani ambazo zinazalishwa na viwanda vyetu vya ndani na kuweza kukidhi viwango vya kuweza kuuzika katika masoko mbali mbali nje ya nchi.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Afya:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa ajili ya Ununuzi, Utengenezaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**06 Disemba, 2023.**

**Raya Issa Msellem**
**KATIBU WA BARAZA.**